KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO-DIVISHENI YA AFRIKA MASHARIKI NA KATI

UNION KONFERENSI YA KASIKAZINI MWA TANZANIA

**IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA**

# KOZI YA KIONGOZI MKUU

**(MASTER GUIDE COURSE)**

PROGRAMU YA KUANDAA VIONGOZI WA VIJANA WADOGO KANISANI

## UFAFANUZI WA UTEKELEZAJI WA MAHITAJI YA MTAALA

(SAHIHISHO LA 2013/17)

**Mtayarishaji**

**Elias Kasika**
Mkurugenzi
Huduma za vijana
Union ya Kasikazini mwa Tanzania
Februari, 2017

**MTAALA WA KIONGOZI MKUU NA UFAFANUZI WA MAHITAJI YA KOZI**

A. UTANGULIZI MKUU- **IELEWE IDARA YA VIJANA KATIKA UPANA WAKE**

Idara hii, ambayo zamani ilijulikana kwa jina la, IDARA YA VIJANA, baadaye ilipata badiliko la jina na kuitwa, IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA. Kusudi la badiliko hili ni kuwafanya wanaojiunga katika Idara hii wajue mapema kuwa ni Idara inayoshughulika na **huduma nyingi,**

(siyo huduma moja), kama matokeo ya aina za watu wanaohudumniwa na Idara hii.

**Je ni akina nani wanaohusika na Idara hii?**
Idara inawahudumia watoto na vijana kuanzia umri wa miaka 6 hadi miaka 35 na wote wanaozidi umri huo wanaopenda kufanya huduma zinazoshughulikia umri huu. Pamoja na kwamba jina linalotumika kuitambulisha Idara ni Vijana, ni kweli bado kuwa wanaohudumiwa wamo watoto katika mgawanyika wa marika kwa kuzingatia ukuaji wa kimwili.Hivyo ni sahihi kusema kuwa Idara ya Vijana inajishughulisha na Vijana walio watoto wadogo; Vijana walio watoto wakubwa; Vijana wadogo wanaopevuka; Vijana wakubwa wanaojiandaa kuanza maisha yao, na Vijana wakubwa waliojitegemea, wawe na ndoa au la. Mchanganyiko huu wa vijana hulazimisha iwepo haja ya kuyatambua makundi ya vijana na kutengeneza mpangomkakati wa kuhudumia kila kundi la vijana. Na kwa sababu makundi yanayohudumiwa ni mengi, ndiyo sababu jina la Idara likawa, **Idara ya Huduma za Vijana**. Makundi makubwa ya kimarika yanayohudumiwa na Idara hii ni mawili: (a) Vijana wadogo-(miaka 6-15), na (b) Vijana wakubwa-(16-30++).

**Vijana wadogo nao wamegwanywa katika makundi makubwa mawili**

a. **Wavumbuzi- Umri wa 6-9.** Wameanza kutoka mikononi mwa wazazi kwa kuanza shule. Wengine hupelekwa shule za bweni ijapokuwa ni wadogo sana usiotakiwa kukaa mbali na wazazi kwa kipindi kirefu, wakati wengine husoma shule za kutwa kwa kushinda mbali na wazazi wakiwa chini ya uangalizi wa waalimu na kuambukizwa mazoea mapya na marafiki waliowapata shuleni.
b. **Watafuta Njia- Umri wa miaka 10-15**. Umri huu una makundi mawili ya vijana wadogo: (1) Watoto wakubwa, (10-12). Hili kundi linatakiwa kuandaliwa kukabiliana na mabadiliko katika makuzi ya kimwili, yanayolikabili miaka michache mbele kama matokeo ya mwanzo wa kubarehe; (2) Vijana wadogo, (13-15). Ni kundi la pili linalopitia mabadiliko mengi mwilini kama matokeo ya kubarehe, ambayo halielewi jinsi ya kukabiliana nayo, likihitaji msaada wa mtu mzoefu au mwenye ujuzi huo. Makundi yote mawili yanahitaji maongozi ya karibu toka kwa mzazi au mlezi au mwalimu aliyejielimisha katika kuwahudumia. Pamoja na mabadiliko mwilini, rika zote mbili, yaani, Wavumbuzi na Watafuta Njia, zinahitaji malezi ya kiroho, yanayotolewa na mtu aliyeandaliwa vizuri kuwakuza kiroho na kimaadili.

**Vijana wakubwa nao wamegawanyika makundi makubwa mawili**

a. **Mabalozi, umri wa 16-21, (Vijana Wakubwa wanaopitia Kupevuka)**. Kupevuka kimwili kunakosemwa hapa kunaanzia umri wa miaka 16 - 19 au 20. Kimakuzi kundi hili lina miili mikubwa na nguvu nyingi zaidi zinazotakiwa kuelekezwa ili zitumike kwa faida na sio kwa hasara, kwao na kwa jamii kwa ujumla. Nguvu hizi zisipoelekezwa vizuri umri huu huathirika kwa kushindwa kujenga msingi imara kwa maisha ya mbele. Waalimu wa rika

hili huhitaji mafunzo maalumu ili kuwawezesha kuelekeza jinsi ya kuoanisha matumizi ya nguvu miilini na ujenzi wa tabia na maadili mema. Mwalimu wa kundi hili ni tofauti na mwalimu wa vijana wdogo tuliomaliza kuwajadili, wa umri wa miaka 6-15.

b. **Vijana Wakubwa wanaokomaa, (umri 22-30++).**
Kundi hili hukabiliana na utambulisho wa kijinsia na kihadhi. Wengi wao wanataka kuoa/kuolewa, hivyo hujishughulisha kuvuta usikivu wa jinsia nyingine kwa juhudi zote. Wakati huo huo bado wako wasiojitegemea kimaisha, wengine wakiwa ni wanafunzi bado, wakti wengine wakiwa hawajaamua kazi yao ya maisha. Wengine kwa kukosa mashauri hujikuta wanaingia katika suala la ndoa mapema, kisha kujikuta katika migogoro inayosababisha wajaribiwe kujiondoa katika ndoa. Kiongozi anahitajika wa kusaidia kundi hili la vijana wakubwa, kuwashauri na kuwaongoza, maan mara nyingi vijana wa umri huu, kwa kukosa mashauri ya mapema hujikuta wakichukia maisha yao ya siku za mbele kwa kujutia wanachopitia, ambacho ni uzoefu mchungu. Waalimu wa kundi hili, sawa na rika la mabalozi, ni wenye elimu tofauti na waalimu wanaohudumia umri wa miaka 6-15, yaani wanaohudumia Wavumbuzi na Watafuta Njia.

**<u>Nani awahudumie vijana kwa kuzingatia rika zilizotajwa?</u>**

Jibu rahisi kwa swali la ni nani awahudumie vijana kwa kuzingatia rika ni kwamba ni yule mwenye mafunzo ya kufanikisha huduma hiyo. Hoja ni kwamba anapataje mafunzo hayo?
Idara ya Vijana hushughulika na aina mbili kuu za huduma:

1. Kuandaa Viongozi wa vijana kupitia mitaala iliyoandaliwa,
2. Kuwalea vijana kiroho na kuwaongoza kumtumikia Mungu wao kwa njia ya Kanisa.

**Kozi mbili hutumika kuandaa viongozi wa vijana kanisani:**

1. **Kiongozi Mkuu-** huandaa viongozi wa kuwahudumia vijana wadogo, yaani Wavumbuzi na Watafuta Njia. Vijana hawa huhudumiwa kanisani kwa kutumia vyama viwili: (1) Chama cha Wavumbuzi na (2) Chama cha Watafuta Njia. Kwa faida ya kurahisisha umoja wa wanaofundishwa kuongoza vijana hawa, Chama cha Master Guide Club chaweza kuundwa kwa kutegemeana na wingi wa wanaofundishwa na wfundishaji, lakini sio kwamba ni hitaji la muundo wa Idara, bali hushauriwa hivyo inapoonekana itaboresha ufanisi wa huduma.

2. **Kiongozi Mwadventista**-(Youth Leadership Master), huandaa viongozi wa vijana wakubwa, yaani Mabalozi na Vijana Wanaokomaa, (Young Adults). Vijana hawa huhudumiwa kanisani kwa kutumia vyama viwili vilivyo tofauti: (1) Mabalozi, (4) Vijana wakubwa**.** Chama cha Youth Leadership Master chaweza kuundwa kwa kutegemeana na wingi wa wanaofundishwa na wfundishaji, lakini sio kwamba ni hitaji la muundo wa Idara, bali hushauriwa hivyo inapoonekana itaboresha ufanisi wa huduma.

3. **Muhimu Kujua Kumhusu Kiongozi Mkuu**, (Master Guide). Akitumika kuongoza Vijana wakubwa, iwe ni Mabalozi au Vijana Wanaokoma, anawaongoza bila Taaluma itakiwayo. Hujikuta akitumia karama za Roho au Talanta zaidi, lakini siyo mafunzo rasmi yaliyoandaliwa na Idara. Hivyo inapotokea ameshindwa kuleta matunda yaliyo kusudiwa uelewa huu uwe akilini mwa wanaomfanyia tathmini, maana hutumika bila ujuzi. Kwa upande wa kinyume, Kiongozi Mkuu, (Master Guide) aliye na pini ya kudhihirisha kuhitimishwa mfunzo akishindwa kuwahudumia Vijana wadogo, (6-15), hapo inabidi uwepo ufuatiliaji wa karibu wa nini kimetokea. Mambo kadhaa itabidi yafuatiliwe miongoni mwake yakiwemo haya: (1) Nani alikuwa mwalimu wake? (2) Amejifunzia wapi? (3) Amejifunza kwa muda gani? (4) Ni nani aliyethibitisha kuhitimishwa kwake?

B. **<u>YAELEWE MABADILIKO KATIKA MTAALA WA KOZI YA KIONGOZI MKUU</u>**

Kadri uongozi wa Idara ya Huduma za Vijana wa Divisheni unavyozunguka toka Union moja hadi nyingine, na toka Konferensi moja ndani ya Union hdi nyingine, imegundulika kuwa Makadi yanayotumika kuwafunza wanafunzi wa Kozi ya Kiongozi Mkuu yanakuwa tofauti, mengi yakiwa ni ya zamani sana yaliyopitwa na wakati kwa mujibu wa maboresho yanayofanywa na Makao Makuu ya Kanisa kadri miaka inavyopita na katika kukabiliana na changamoto za kuwahudumia vijana toka kizazi hadi kizazi. Kwa takribani miaka 11, kuanzia 2002 hadi 2013, Mtaala wa Kozi ya Kiongozi Mkuu umelazimika kupitia masahihisho mara 2, yaani sahihisho la mwaka 2012 na sahihisho la mwaka 2013, kutokana na sababu za kiutendaji zaidi. Kadi la Mahitaji ya Kiongozi Mkuu tutakalotumia kuanzia Feb 2017, litatofautiana kidogo na sahihisho la 2013, kutokana na mambo matatu muhimu. La kwanza ni kwamba Kanisa ni moja ulimwenguni na hivyo mahitaji yanatakiwa kufanana duniani kote. Katika union yetu kadi letu, (ambalo ni sahihisho la 2013), mahitaji machche yameunganishwa, aidha kuliacha hitaji la mwisho la kuandaa Jarida la Taarifa ya mafunzo. La pili ni umuhimu wa kulishirikisha kanisa mahalia katika mafunzo ya kumwandaa mwanafunzi wa Kozi ya Kiongozi Mkuu, ambaye hutakiwa kujifunza akiwa kanisani mwake, yaani kanisa lake liwe ndilo kituo cha mafunzo, badala ya mwanafunzi kujifunzia katika vituo vinginevyo. La tatu na la mwisho ni kwamba Mkurugenzi wa Union kwa sasa anatakiwa kushiriki katika kuidhinisha kuhitimu kwa

mwanafunzi. Hitaji hili limetakiwa lionyeshwe kwenye kadi la sasa. Kinachoelezwa hapa chini ni maelekezo ya Divisheni yetu, tunayotakiwa kufanyia kazi, yaliyotolewa wakati wa Mkutano wa Uongozi uliofanyika Kisumu, Feb 6-11, 2017. Sambamba na maelekezo haya Mahitaji ya Kadi nayo yametolewa upya kwa kuzingatia marekebisho na maboresho yaliyofanywa na Divisheni na GC.

a. <u>Maelekezo ya kuboresha mafunzo ya Kiongozi Mkuu.</u>

1. Mwanafunzi wa kufundishwa kozi hii ya Kiongozi Mkuu hupendekwa na Kanisa lake kwa maandishi ya vikao halali vya kanisa.
2. Kabla ya kuona muhuri wa Kanisa na sahihi ya kiongozi husika, mchungaji au mzee wa Kanisa mafunzo hawezi kuanza.
3. Mafunzo hufanyikia kanisani kwa mwanfunzi sio nje ya kanisa lake, eti katika kituo kilichochaguliwa na wakufunzi. Hii ni kwa sababu mafunzo mengi yanahusisha matendo ambayo mwanfunzi hutegemewa kuyafanyia kanisani kwake.
4. Mkurugenzi wa Konferensi ndiye huchagua waalimu wa kuwafunza wanafunzi, ambao kwa kawaida ni Master Guide walio kazini na wenye uwezo wa kufunza wengine. Katika baadhi ya mafunzo ya vitendo Mkurugenzi huweza kumtaka Mchungaji au Mzee wa Kanisa au Mshauri wa Vijana, kumpatia mwanafunzi majukumu, kuyasimamia na kuona yalivyokamilishwa kisha kutia sahihi yake kwenye Kadi.
5. Katika mafunzo haya hatutegemei kuona mtihani mmoja kwa kozi nzima maana hatuna mwongozo wala mtaala unaodai kitu hicho, bali mtihani mmoja kwa kipengele kimoja huo ni sawa, uwe ni ni kuandika au wa kutenda. Urasimu hautegemewi kuonekana kuchelewesha mafunzo au kuhitimu. Tunalinda vyote viwili, ubora na uzuri kwa uwiano mzuri.
6. Kwa kuwa yapo mahitaji yanayomtaka mwanafunzi kufunsdisha darasa la Wavumbuzi au Watafuta Njia hadi wavishwe pini, hatutegemei kumwona akivishwa pini yeye kwanza kabla ya kuona uvishaji wa wanafunzi wake.
7. Inapendekeza zaidi kuwaona wanfunzi wa Kozi wa Kiongozi Mkuu wakipatikana wenye umri kati ya 16 -18 badala ya kuwa na wengi wanaovishwa waliozidi umri wa miaka 30, ambao wanaonekana kuwa wanachama w heshima zaidi.
8. Wanaofundisha mfunzo haya, kwa vijana wdogo au kwa vijana wakubwa, hatutegemei wawe ni watu wa kulipwa mshahara maan huduma za kanisa hufanyika kwa kujitolea siku zote.
9. Miongozo ya mafunzo tunategemea iwe imenunuliwa na Kanisa lenyewe ili itumike kufundishia. Mwanafunzi akipenda kujinunulia nakala zake kwa faida zake binafsi inakuwa ni bora pia. Kukosekana kwa miongozo ya lazima kufundishia kutasabisha mashaka juu ya uwezo wa kutoa huduma kwa upande wa mwanafunzi, kiongozi mtarajiwa.

b. Maelekezo  Maalumu kuhusiana na Kumuhitimisha Mwnafunzi

1. Kipindi cha chini kabisa kukamilisha mahitaji hakitapungua mwaka 1, maana yapo mahitaji yanayodumu kwa mwaka mmoja. Kipindi cha juu ni miaka 3.
2. Kazi iliyofanywa na mwanafunzi itatunzwa katika jarida lake aliloliandaa, kila hitaji likionyeshwa humo jinsi lilivyotimizwa kwa jinsi lilivyohitajika kufanyika. Kipengele hiki imebidi kifanywe moja ya mahitaji ili kupewa uzito unaotakiwa.
3. Ijapokuwa inaruhusiwa kuchukua kozi ya Msingi mojawapo kati ya Wavumbuzi na Watafuta Njia, mashauri ya uongozi ni kwamba mwanafunzi achukue kozi zote ili awe na uwezo mzuri wa kutoa huduma kwa makundi yote mawili.
4. **Ni muhimu Kumbuka kuwa:** Ili tuokolewe hatugharimiki kwa lo lote, maana ni kwa neema yake Yesu peke yake, (Efe2:8); lakini ili tuwe wanafunzi wake Yesu, kwa kumjua Mungu na kumwamini tunagharimika kila kitu. Tafakari Luke 14:26,27,33. Ni katika muktadha huu mwanafunzi wa Kozi ya Kiongozi Mkuu huhitajika kutoa muda wake na nguvu zake, kushughulikia wokovu wake na wa wenzake, na hasa vijana wadogo waliowekwa chini ya dhamana yake.

C. **BAADA YA MWANAFUNZI KUHITIMISHWA**

Wengi wanaohitimu Kozi ya Kiongozi Mkuu hudhani hakuna kujielimisha tena baada ya hapo. Ijapokuwa ni kweli kwamba Master Guide ndiyo kozi kiini ya uongozi wa vijana wadogo kanisani, bado ni kweli pia kwamba kuna kozi zingine mbili anazotegemewa kuchukua mbele ya safari ili kujiongezea ujuzi kazini. Kwa majina ya zamani Kozi hizi ziliitwa: (1)Pathfinder Leadership Award, (PLA) na (2) Advanced Pathfinder Leadership Award, (APLA).  Kwa sasa kuna badiliko la jina la Kozi. Kozi inaitwa **AYMT – Adventist Youth Ministry Training**.

D. **VIAMBATANISHO KUELEZEA UTEKELEZAJI WA MTAALA:**

1. **MAHITAJI YA KOZI- SAHIHISHO LA 2016 – Rejea Kiambatanisho- 1**
2. **UFAFANUZI WA MAHITAJI- Rejea Kiambatanisho- 2**
3. **FOMU YA TAARIFA YA HUDUMA KILA ROBO- Kiambanisho-3**

**KIAMBATANISHO- 1**

**MAHITAJI YA KOZI- KIONGOZI MKUU- SAHIHISHO LA 2013**

# I. MASHARTI YA AWALI

1. Uwe mshiriki wa Kanisa la Waadventista Wasabato aliyebatizwa na mwenye msimamo mzuri .
2. Baraza la Kanisa lako  likushuhudie kwa  kukupendekeza kusomea kozi hii kwa maandishi.
3. Umri wako usipungue miaka 16 unapoanza kozi hii na usipungue miaka 18  unapohitimishwa
4. Uwe unatumika katika Chama cha Wavumbuzi au Watafuta njia

kama muhudumu mwenye bidii.

5. Ukamilishe Kozi ya Msingi mojawapo na utumike ndani ya chama kimojawapo kwa muda usiopungua mwaka mmoja.
    1) Huduma za Wavumbuzi
    2) Huduma za Watafuta Njia

**II. KUJIENDELEZA KIROHO**

1. Soma au sikiliza ukisomewa Kitabu cha "NJIA SALAMA" na ufanye ufupisho wa ukurasa mmoja kueleza ulivyonufaika na ulichosoma.
2. Kamilisha ibada ya maombi binafsi ukitumi mwongozo uitwao, "Kristo Aliye Njia" (Christ The Way), au utaratibu ulioidhishwa

   wa Usomaji wa Vitabu 4 vya Injili. pamoja na kitabu cha Tumani la Vizazi.
3. Soma au sikiliza ukisomewa kitabu cha: Tumaini La Vizazi, (Desire of Ages)
4. Fanya mojawapo kati ya yafuatayo hapa chini:
    a. Andaa masomo ya kesha la asubuhi ya wiki zisizopungua nne, ukitumia kalenda ya ubunifu wako mwenyewe, ukifanya muhtasari wa masomo ya kila siku.
    b. Kamilisha hatua za Uanafunzi wa kiroho wa mtu binafsi kwa kusoma Mtaala wa ukuaji wa kiroho uliopendekezwa na Kanisa Makao Makuu(Steps to Discipleship Spirituality Curriculum of GC Youth).
5. Shiriki katika angalao tukio moja la uinjilisti liwe ni kwa njia ya Huduma za jamii au program ya hadhara.
6. Andaa muhtasari wa ukursa 1 kuelezea kila msingi wa Imani kwa misingi 28 ya Imani Ya Kanisa la Waadventista Wasabato, ukorodhesha mawazo yaliyo kiini cha huo msingi,( point form**)**
7. Dhihirisha ufahamu wako wa Misingi ya Imani kwa kuandaa kwa kina na kuelezea misingi 4 kati ya ifuatayo:(a). Uumbaji, (b) Uzoefu wa Wokovu, (c) Kukua Katika Kristo, (d) Masalio na Utume wake, (e) Ubatizo, (f) Karama za Roho na Utume, (g) Karama ya unabii, (h). Sabato,(i) Huduma ya Kristo katika Hekalu la Mbinguni, (j) Kuja kwa Kristo Mara ya Pili (k). Kifo na Ufufuo.

   **Msingi uliochaguliwa – Jina na Utekelezaji wake**:

1) ________________________________________________________________

2) ________________________________________________________________

3) ________________________________________________________________

4) ________________________________________________________________

8. Ongeza ujuzi wako wa urithi wa Kanisa kwa kukamilisha yafuatayo:

a) Pata Tuzo ya Urithi wa Kanisa la Waadventista Wasabato.

b) Soma kitabu kitabu kinachoelezea Huduma za Vijana za Kanisa la Waadventista Wasabato kama :

- The Pathfinder Story kilichoandikwa na Robert Holbrook, au
- "We are the Pathfinder Strong Strong", kilichoandikwa na Willie Oliver na Patricia Humprey
- Kitabu kinginecho kinachoelezea sehemu ya Historia ya Kanisa ambayo hujaisoma, kilichoidhinishwa na Union/ Konferensi yako.

c) Soma Kitabu kinachozungumzia historia ya Kanisa, kama vile:

1) Anticipating the Advent by George Knight.
2) Tell It to the World by Mervyn Maxwell
3) Light Bearers to the Remnant by Richard W Schwarz and Floyd Greenleaf
4) The Church Heritage Manual produced by the General Conference Youth Department.
5) Kitabu kinginecho kilichoidhinishwa na uongozi katika Union au Konferensi yako.

9. Hudhuria semina au fanya utafiti kisha kwa maandishi yasiyopungua kurasa 2 juu ya uchambuzi wa silika za watu wenye majumuisho ya silika za aina nyingi.

**III. KUJIENDELEZA KATIKA STADI MBALI MBALI**

1. Hudhuria na ukamilishe semina isiyopungua dakika 90 katika kila somo miongoni mwa masomo 12 yafuatayo:
   a. **Stadi za Uongozi**
      1) Jinsi ya kuwa kiongozi wa Kikristo
      2) Njozi, Utume na Motisha
      3) Kukabiliana na hatari zitokanazo na huduma za Wavumbuzi na Watafuta Njia
      4) Nidhamu
   b. **Stadi za Mawasiliano**
      1) Dhana ya Mawasiliano na kusikiliza
      2) Mawasiliano ya ana kwa ana
      3) Kuielewa mitindo ya kufundishia
   c. **Ubunifu na Vitendea Kazi**
      1) Jinsi ya kuandaa ibada yenye mguso
      2) Kuelewa na kutumia ubunifu
   d. **Uinjilisti wa Watoto**
      1) Kanuni za uinjilisti wa vijana na watoto
      2) Jinsi ya kumuongoza mtoto kwa Kristo
      3) Kuzingundua karama zako za Roho
2. Pata au uwe na Nishani zifuatazo:
   a) Masimulizi ya kikristo
   b) Stadi za Ukambikaji , hatua ya 1-IV
   c) Elimu ya Msingi juu ya Kwata na Parade
   d) Mafundo
3. Pata Nishani mbili zaidi au Tuzo mbili zaidi za uchaguzi wako ambazo ulikuwa hujapata huko nyuma.
4. Pata cheti cha wakati huu cha msaada wa kwanza, cha Red Cross, au Cheti cha Usalama, (Safety Certificate) au huduma inayotimiza hitaji hilo.
5. Kwa kipindi kisichopungua mwaka moja shiriki kusimamia huduma vijana wadogo katika darasa mojawapo la Wavumbuzi au Watafuta Njia au fundisha darasa la Shule ya Sabato kwa watoto wa umri wa miaka 6-15.

## IV. MAENDELEO YA MTOTO

1. Soma au usomewe kitabu cha: “Education”, (Elimu ya Kweli)cha E.G. White, na uandike na kukabidhi ufupisho wa ukurasa mmoja wa mambo uliyonufaika nayo kutokana na usomaji huo.
2. Soma au usomewe kitabu kingine juu ya maendeleo ya mtoto,kati ya Child Guidance, au Messages to young People vyote vya E.G White, na uandike na kukabidhi ufupisho wa

ukurasa mmoja wa mambo uliyojifunza na jinsi ulivyonufaika nayo.

3. Hudhuria semina tatu zinazojadili maendeleo ya mtoto wa umri unaohudumia, au semina za kielimu zihusianazo na umri halisi wa mtoto unashughulika naye.
4. Kwa muda wa masaa 2 chunguza shughuli zifanywazo na Wavumbuzi au Watafuta Njia na uandike ulichooona kutokana na shughuli walizofanya wao kwa wao na miongoni mwao na waalimu wao.

## V. KUJIENDELEZA KATIKA UONGOZI

1. Soma kitabu kinachozungumzia kujiendeleza katika stadi za uongozi katika ujumla wake cha uchaguzi wako miongoni mwa orodha iliyopendekezwa hapa:
   a. Positive Church in a Negative World, John Arrias

   b. Take the Risk, Ben Carson
   c. Ellen White on Leadership by Cindy Tutsh
   d. Help! I’m being followed by Clinton Valleyn
   e. Other book recommended by your Conference/ Mission, Youth Ministries Director.

2. Dhihirisha kuwa na stadi zako za uongozi kwa kufanya yafuatayo:
   a) Andaa na uendeshe ibada 3 kwa watoto na au vijana wanaobarehe, za ubunifu wako mwenyewe.
   b) Shiriki katika Kambi la Vijana ngazi ya Konferensi, wewe ukiwa na watoto wa kanisani kwako ukitumika kama kiongozi wao.
   c) Fundisha tuzo tatu za Wavumbuzi au Nishani mbili za Watafuta Njia
   d) Saidia katika kupanga na kuongoza safari ya mafunzo ya Wavumbuzi, Watafuta Njia au darasa la Shule Sabato lenye umri kati ya miaka 6-15, iliyofanyikia nje ya Kanisa
   e) Uwe miongoni mwa maofisa wachapa kazi wa Chama cha Wavumbuzi, Watafuta Njia, au wa shule ya sabato, kwa mwaka mmoja na uhudhurie angalau asilimia 75 ya mikutano ya viongozi.
3. Andika malengo yako makuu unayohitaji kuyatimiza katika huduma yako.
4. Tambua majukumu matatu ya sasa katika maisha yako,mojawapo likiwa ni la kiroho kisha kwa kila jukumu

orodhesha malengo madogo 3 unayotaka kufanikisha.

**VI. KUJIENDELEZA KIAFYA**

1. Kuza afya ya viungo vyako kwa kukamilisha mojawapo ya yafuatayo:
   a) Kamilisha tuzo ya AY ya Silver Award na kama unayo tayali, kamilisha tuzo ya AY ya Gold Award, zote zikihusika na mazoezi ya viungo
   b) Shiriki katika programu ya mazoezi ya viungo iliyoandaliwa na shule.
   c) Shiriki katika mpango maalumu wa mazoezi ya viungo uliouchagua kwa kuongozwa na kitabu cha mazoezi ya viungo, chini ya ushauri wa msimamizi wa mafunzo yako.

**VII. TAARIFA YA MAFUNZO – DOCUMENTATION**

1. Kwa ajili ya uhakiki wa mafunzo, Andaa na kabidhi Jarida (Portifolio), kuonyesha kila hitaji lilivyotimizwa kwa kuzingatia mahitaji yalivyoelekeza na jinsi lilivyofanyika.

**UTHIBITISHO WA KUKAMILISHA MAHITAJI – NGAZI YA KANISA NA KONFERENSI**

Nathibitisha kwamba: ____________________________ alianza Kozi ya Kiongozi Mkuu tarehe ________
Amekamilisha mahitaji yote tarehe: __________________

1. Mwalimu wa Kozi: ________________________________________ Tarehe: _____________________
2. Kiongozi wa Vijana Kanisani: _______________________________ Tarehe: _____________________
3. Mkurugenzi wa vijana wa Konf. _____________________________ Tarehe: _____________________

**IDHINI YA KUHITIMISHWA MWANAFUNZI – NGAZI YA UNION**

Baada ya Ukaguzi wa Jarida la Mafunzo ya mwanafunzi, na kwa taratibu zingine za kiofisi, Pendekezo:

________________________________________________

________________________________________________

Mkurugenzi wa Vijana Union: Jina____________________Sahihi___________ Tarehe_______

**KIAMBATANISHO- 2**

**KIONGOZI MKUU - UFAFANUZI WA MAHITAJI YA KOZI**

## I. MASHARTI YA AWALI

1. **Uwe mshiriki wa Kanisa la Waadventista Wasabato aliyebatizwa na mwenye msimamo mzuri**
    - Asiye mshiriki wa kanisa au mshiriki aliye chini ya nidhamu ya kanisa haruhusiwi kuchukua majukumu ya uongozi wa kanisa. Mwanafunzi wa sekondari au vyuoni aliye mbali na kanisa lake, aliye na barua ya kumshuhudia kutoka katika lake anaweza kuidhinishwa na kanisa linalomlea kuchukua kozi hii.
    - Mtindo wa maisha wa mwanfunzi wa Kozi uwe ule wa kuonyesha kumwadhimisha Kristo katika mwili wake, kwa maisha yake na inapobidi kwa mauti yake. Mtu anayependelea kuishi sawa sawa na kawaida za ulimwengu huu hatakuwa miongoni mwa wanaopendekezwa kuongoza wenzake.
2. **Baraza la Kanisa lako likushuhudie kwa kukupendekeza kusomea kozi hii kwa maandishi.**
    - Kabla sahihi ya mchungaji au afisa wa kanisa aliyeidhinishwa hajasaini kadi la mwanafunzi na kugonga muhri wa kanisa, mafunzo hawezi kuanza kwake. Hivyo hitaji hili ndilo ufunguo wa mafunzo.
    - Kwa kuwa sahihi ya mchungaji ndiyo ufunguo wa mafunzo, inabidi kanisa ndilo linunue na kutunza makadi ya Kozi ya Kiongozi Mkuu.
    - Ushuhudiaji huu humaanisha kuwa ili mwanfunzi huyu

ahitimu kozi hii Kanisa, kwa kutumia Baraza lake, litampatia mwanafunzi fursa za kutimiza matakwa yote ya kozi yanayomtaka atumike katika nyadhifa mbalimbali kanisani kwa kipindi kilichotajwa.

3. **Umri wako usipungue miaka 16 unapoanza kozi hii na usipungue miaka 18 unapohitimishwa**
   - Matarajio ya mwalimu ni kwamba mwanafunzi baada ya kufikisha miaka 15, kwa kuwa ndani ya kanisa kama Mtafuta Njia, mwaka wa 15 anakuwa amehitimu pia darasa la Kiongozi.
4. **Utumike katika Chama cha Wavumbuzi au Watafuta njia kama muhudumu mwenye bidii**.
   - Mtu asiye na moyo wa kufanya kazi na watoto hawezi kufanikisha malezi yao.
   - Mtu mwenye moyo wa kuwahudumia watoto huonekana akijihusisha katika program mbalimbali zinazohusu watoto.
   - Pendekezo la Kanisa kumuidhinisha kuchukua kozi ya uongozi huu ni kwa sababu limeona moyo wake wa kupenda kuwahudumia watoto
5. **Ukamilishe Kozi ya Msingi ya Wavumbuzi au Watafuta Njia na utumike ndani ya chama kimojawapo kwa muda usiopungua mwaka mmoja.**
   - Kozi hii, ambayo huchukua masaa 10 ni ya lazima kabla mwanafunzi hajakabidhiwa jukumu la kufundisha darasa lo lote la vijana wadogo.
   - **Kozi ya Msingi ya Watafuta Njia ina vipengele 11, au 12 kama elimu ya UKIMWI**.
     1) Historia, Falsafa na Makusudi ya chama cha Watafuta Njia
     2) Kuwaelewa Watafuta Njia
     3) Uongozi wa Chama
     4) Muundo wa Chama
     5) Mipango na Programu za Chama
     6) Huduma ya Kueneza Imani (Outreach Ministry)
     7) Ufundishaji wa Mtaala wa Watafuta Njia
     8) Ukambikaji na shughuli za nje ya nyumba
     9) Kwata na Sherehe za Chama
     10) Kuwaongoza Vijana wanaopevuka
     11) Huduma za Wavumbuzi
     12) **Elimu ya Kujiepusha na UKIMWI**

- Kozi ya Msingi ya Wavumbuzi ina vipengele 9 au 10 kama elimu ya UKIMWI kitaongezeka:
    1) Historia, Falsafa na Makusudi ya Chama cha Wavumbuzi
    2) Kuwaelewa Wavumbuzi
    3) Uongozi wa Chama
    4) Muundo wa Chama
    5) Programu za Chama
    6) Ufundishaji wa Mtaala wa Wavumbuzi
    7) Wazazi na Huduma za Wavumbuzi (Adventurer Family Network Program)
    8) Tuzo za Wavumbuzi na Ufundishji wake (Adventurer Awards)
    9) Huduma za Watafuta Njia (Pathfinder Ministries)
    10) **Elimu ya kujiepusha na UKIMWI**
- Miongozo ya Kozi hii ambayo hutumiwa na mwanafunzi inunuliwe na kanisa na kuwa mali ya kanisa kwa ajili ya wanafunzi watakaofundishwa baadaye.
- Mkufunzi wa Kozi hii ni Mkurugenzi wa Vijana wa Konferensi, ijapokuwa anaweza kuidhinisha wakufunzi wenza wa kutumika pamoja naye au kwa niaba yake, uwajibikaji ukibakia kuwa ni wa kwake.

**II. <u>KUJIENDELEZA KIROHO</u>**

1. **Soma au sikiliza ukisomewa Kitabu kiitwacho "NJIA SALAMA" na ufanye ufupisho wa ukurasa mmoja kueleza ulivyonufaika na ulichosoma**
    - Kitabu hiki kidogo kinamsaidia msomaji kugundua mchakato wa wokovu kwa njia ya Kristo jinsi ulivyo, kupitia uanafunzi. Idara ya vijana, katika misukumo yake maneno mawili makuu ni: WOKOVU na UTUMISHI. Ni muhimu kwamba mwanafunzi wa Kiongozi Mkuu aielewe dhana hii ya wokovu mapema mwanzoni mwa mafunzo yake.
    - Kabla ya kuelezea **ulivyonufaika** na ulichosoma eleza utangulizi mfupi kuhusu kitabu: (a)Jina la Kitabu, (b) Mwandishi wake na (c) Kusudi la mwandishi. Haya yawe ndani ya aya moja. Aya zinazofuata zigawanywe katika aya ndogo ndogo kuelezea **jinsi ulivyonufaika na ulichosoma**, **ukijihadhali kutokurudia maneno ya uandishi wa kitabu**

**kile katika ukurasa wako mmoja.**

2. **Kamilisha ibada ya maombi binafsi ukitumi mwongozo uitwao, "Kristo Aliye Njia" (ChristThe Way), au utaratibu ulioidhishwa wa Usomaji wa Vitabu 4 vya Injili pamoja na kitabu cha Tumani la Vizazi.**
   - Ijapokuwa ziko program mbalimbali zitumikazo kukua kiroho kwa kujifunza Biblia ambazo hutangazwa na Konferensi zetu, hii program ya Kristo Aliye Njia inayotumika kwa mwaka mzima, ni maalumu kwa Idara ya Vijana ili kumpitisha mwanafunzi katika ujuzi wa Injili jinsi ilivyo na inavyotakiwa kuhubiriwa, wakati huo huo akikua kiroho binafsi.
3. **Soma au sikiliza ukisomewa kitabu cha: Tumaini La Vizazi, (Desire of Ages**)
   - Kitabu cha Tumaini la Vizazi, kilichoandikwa na Ellen White, kinaelezea maisha ya Yesu. Kwa kukisoma au kusomewa mtu hupata uelewa wa Yesu ni nani na alichofanya kwa ajili ya wanadamu wenye dhambi. Pamoja na ukweli kwamba vitbu vinne vya Injili vinamwelezea huyu Yesu, lakini hapa mwanafunzi hutakiwa kumweleza huyu Yesu kupitia Maandiko ya Unabii, ya Ellen White. Taarifa ya ukurasa 1 inaweza kutoa muhtsari wa kilichoeleweka endapo mtu anaulizwa kumwelezea huyu Yesu kwa maneno machache. Muhtasari huu uguse maeneo yote muhimu.
4. **Fanya mojawapo kati ya yafuatayo hapa chini**:
   f. Andaa masomo ya kesha la asubuhi ya wiki zisizopungua nne, ukitumia kalenda ya ubunifu wako mwenyewe, ukifanya muhtasari wa masomo ya kila siku.
   g. Kamilisha hatua za Uanafunzi wa kiroho wa mtu binafsi kwa kusoma Mtaala wa ukuaji wa kiroho uliopendekezwa na Kanisa Makao Makuu(Steps to Discipleship Spirituality Curriculum of GC Youth)
   - Katika maduka ya vitabu kuna vitabu vingi vilivyoandikwa na watu ili vitumike kama kasha la asubuhi vyenye majina mbalimbali. Wakristo wengi huamua kununua hivyo na kujisomea kila asubuhi. Swali ni kwamba kwa nini usiandike kitabu chako mwenyewe angalao cha kutumika kwa miezi mitatu tu?
   - Hitaji hili linakupatia uzoefu wa kujiandikia kesha lako

mwenyewe kwa njia iliyo rahisi sana. Jiandalie daftari dogo na kila siku utumie ukurasa mmoja wa kujiandikia kesha lako kwa utaratibu huu: (a) Tarehe_____ (b) Fungu ulilosoma katika Biblia(Taja)________ (c) Fungu limekupatia mawazo gani mapya uliyokuwa hauna na unayoenda kufanyia kazi? (Yaeleze)________ (d) Unaamua kuombea nini unachotaka kuona kikitokea katika maisha yako? (Kieleze)__________.

- Ukiona kuwa una ugumu wa kufanikisha uandishi wa kasha lako basi tumia kasha lililopendekezwa na Idara ya Vijana ndani ya Konferensi yako.

5. **Shiriki katika angalao tukio moja la uinjilisti liwe ni kwa njia ya Huduma za jamii au program ya hadhara.**
    - Mungu hutoa mafunuo kwetu kwa njia ya Roho wake Mtakatifu kwa wingi tunapokuwa kazini pamoja naye. Muda tunaotumia kujifunza kweli zake ili tuwashirikishe wengine kuzijua hutumika pia kama muda wa kutuimarisha kiroho. Tunapokwenda kazini pamoja naye hutudhihirishia zaidi jinsi alivyo mwenye enzi kupitia utendaji anaotushirikisha wa kutambua uweza wake, na kutuongezea imani na kukua kiroho.
    - Mchungji wa kanisa au kwa kuwakilishwa na msaidizi wake mzee wa Kanisa wamtengenezee mwanafunzi wa Kozi ya Kiongozi Mkuu fursa hii ya kushiriki tukio la uinjilisti kwa kusimamiwa na wao wenyewe, akitumika kama mwanafunzi mafunzoni.

6. **Andaa muhtasari wa ukursa 1 kuelezea kila msingi wa Imani kwa misingi 28 ya Imani Ya Kanisa la Waadventista Wasabato, ukorodhesha mawazo yaliyo kiini cha huo msingi,( point form) .**
    - Hatuwezi kufundisha tusichojua. Kila msingi wa imani yetu umekusudiwa utumike katika kueneza imani yetu na kutuimarisha sisi katika imani kwa kuitii kweli ya Neno lake**.**
    - Muhtasari ulio katika Kanuni ya Kanisa hutumika kuelezea uelewa wa kanisa kuhusu misingi hiyo. Unapofundisha mawazo au kweli zilizo katika muhtasari huo usiachwe kuelezwa.
7. **Dhihirisha ufahamu wako wa Misingi ya Imani kwa kuandaa**

**kwa kina na kuelezea misingi 4 kati ya ifuatayo:(a). Uumbaji, (b) Uzoefu wa Wokovu, (c) Kukua Katika Kristo, (d) Masalio na Utume wake, (e) Ubatizo, (f) Karama za Roho na Utume, (g) Karama ya unabii, (h). Sabato, (i) Huduma ya Kristo katika Hekalu la Mbinguni, (j) Kuja kwa Kristo Mara ya Pili (k). Kifo na Ufufuo** .

- Misingi ya Imani iliyo orodheshwa hapa ndiyo muhimili unaolitofautisha Kanisa la Waadventista Wasabato na makanisa mengine. Misingi hii inaelezwa na Kanisa la Waadventista Wasabato kwa namna ambayo madhehebu mengine hayaelezi. Pamoja na kwamba mwanafunzi huombwa kuandika kuelezea misingi 4 kati ya hii, bado anawajibika kujua na kuelezea mmoja mmoja kwa usahihi, mana hategemewi kuendesha mahubiri ya hadhara bila kufundisha misingi hii yote.
- Soma kitabu cha Misingi ya Imani yetu kiitwacho, "Seventh-day Adventist beliefs" au Fundamental beliefs kinachoelezea teolojia ya misingi ya imani yetu. Kitabu hiki kinapatikana kwa Kiswahili katika maduka ya vitabu ABC kwa jina la Misingi ya Imani. Hicho kitakupa ufahamu utakaotumia kukamilisha hitaji hili.
- Mchungaji na au mzee wa Kanisa waliomfundisha mwanafunzi hadi akafikia hatua ya kubatizwa wanategemewa walimfundisha vema misingi hii. Endapo hawakufanya vema, huu ni wakati wao wa kurudia misingi hii kwake wakimuimarisha katika misingi ya imani na katika kulijua kanisa lake.
- Miongoni mwa misingi 11 iliyoorodheshwa juu mwanafunzi, pamoja na kujifunza vizuri yote, lakini achague misingi 4 atakayoiandikia kwa kina jinsi kanisa linavyoamini kuhusiana na fundisho hilo, akionyesha linavyotofautiana na makanisa mengine.

8. **Ongeza ujuzi wako wa urithi wa Kanisa kwa Kukamilisha yafuatayo**:

   a. **Pata Tuzo ya Urithi wa Kanisa la Waadventista Wasabato**.

   - Kuielewa historia ya Kanisa la Wadventista Wasabato,

jinsi lilivyoanza ulimwenguni, na kusudi lake ni jukumu la kila mshiriki na kila mwanachama wa chama cha vijana.

- Kuielewa historia ya kanisa la Waadventista Wasabato lilivyoanza katika Union, Konferensi, mtaa, na kanisa lako mahalia unakosali kunadhihirisha ukomavu wa kuielewa safari ya imani kwa njia ya Kanisa. Kila mwanafunzi ayakamilishe haya ili awe na uwezo w kuyafundisha kwa wengine.
- Katika Union yetu tumependekeza Kitabu cha Historia ya Kanisa kilichoandikwa na mch Elisha Okeyo ndicho kitumike kulielezea kanisa ngazi ya Union na Konferensi.

b. **Soma kitabu kitabu kinachoelezea Huduma za Vijana za Kanisa la Waadventista Wasabato kama** :

- The Pathfinder Story kilichoandikwa na Robert Holbrook, au
- "We are the Pathfinder Strong Strong", kilichoandikwa na Willie Oliver na Patricia Humprey
- Kitabu kinginecho kinachoelezea sehemu ya Historia ya Kanisa ambayo hujaisoma, kilichoidhinishwa na Union/ Konferensi yako.

h. **Soma Kitabu kinachozungumzia historia ya Kanisa , kama vile**:

1. Anticipating the Advent by George Knight.
2. Tell It to the World by Mervyn Maxwell
3 Light Bearers to the Remnant by Richard W Schwarz and Floyd Greenleaf
4 The Church Heritage Manual produced by the General Conference Youth Department.
5. Kitabu kinginecho kilichoidhinishwa na uongozi katika Union au Konferensi yako.

- Ni muhimu kwa kila mwanafunzi wa Kiongozi Mkuu kupata uelewa sahihi wa Kanisa la Waadventista Wasabato kiulimwengu: Jina lake ni lipi? Kwa nini? Lilianza lini? Wapi? Waanzilishi ni akina nani? Kwa nini lianze wakati makanisa mengine ya kikristo tayali yalikuwepo mengi? Vitabu vilivyotajwa hapo juu vinajibu maswali haya.
- Mwanafunzi pia anategemewa aeleze historia ya Kanisa la

Waadventista Wasabato katika Union yake, Konferensi yake, Mtaa wake, nay a kanisa lake mahalia, akilenga kujibu maswali yale yale yaliyoulizwa katika kipengele cha juu. Atapewa mtihani na kuufanya ndipo ahitimu.

9. **Hudhuria semina au kwa maandishi yasiyopungua kurasa 2 kamilisha utafiti juu ya uchambuzi wa silika za watu wenye majumuisho ya silika za aina nyingi**

- Wanadamu tuna tofautiana katika mihemko, silika, hisia na mambo yafananayo na hayo. Haya yana athari kwa tabia zetu ili tuonekane kama wakali, wapole, wenye huruma, wenye hasira, nk. Wakati mwingine sauti za juu hazimaanishi ukali wa mtu au sauti za chini hazimaanishi upole wa mtu. Kuishi na watu wa silika tofauti tofauti kwa kuvumiliana ni miongoni mwa uwajibikaji unaompasa kiongozi.
- Itakuwa vizuri kuchukua muda kujielimisha pia pia katika vitabu vinavyoelezea hisia, silika, mihemko na jinsi ya kuitambua kadri unavyoendelea na utafiti wako. Mkufunzi wako anaweza kusaidia kujua mahali pa kupata hivyo vitabu.

## III. <u>KUJIENDELEZA KATIKA STADI MBALI MBALI</u>

1. **Hudhuria na ukamilishe semina isiyopungua dk 90 katika kila somo miongoni mwa masomo 12 yafuatayo**:

a. **Stadi za Uongozi**

1. Jinsi ya kuwa kiongozi wa Kikristo
2. Njozi, Utume na Motisha
3. Kukabiliana na hatari zitokanazo na huduma za Wavumbuzi na Watafuta Njia
4. Nidhamu

b.**Stadi za Mawasiliano**

1) Dhana ya Mawasiliano na kusikiliza
2) Mawasiliano ya ana kwa ana
3) Kuielewa mitindo ya kufundishia

c. **Ubunifu na Vitendea Kazi**

1) Jinsi ya kuandaa ibada yenye mguso
2) Kuelewa na kutumia ubunifu

d. **Uinjilisti wa Watoto**

1) Kanuni za uinjilisti wa vijana na watoto
2) Jinsi ya kumuongoza mtoto kwa Kristo
3) Kuzingundua karama zako za Roho

- Masomo 12 ya semina yaliyo orodheshwa hapa juu katika

mada aina 4 tofauti kila kundi la mada likiwa na msisitizo wake. Hakikisha unaelewa utofauti wa mada hizi na jinsi kwa pamoja zinavyojazilizana katika uelimishaji. Ni muhimu pia kutaja kuwa huko nyuma masomo hayakuwa 12 bali 8, kisha 10 na sasa ni 12.

- **Chini ya Stadi za Uongozi** lengo ni kugundua kanuni za msingi zitumikazo kuongoza kikundi au vikundi vya watu ili kufanikisha malengo yaliyokusudia. Kanuni za msingi zinazofundishwa huwa ni zile zinazoakisi uongozi wa Yesu Kristo na jinsi alivyofanya kuwafanya watu wamuamini na kumfuata. Watu hawawezi kumfuata Mtu asiye jua aendako na afanyacho. Utume wako kwao unatakiwa kuelweka dhahiri. Kiongozi aeleweke makusudi yake na jinsi anavyotaka yafanikishwe na timu anayoiongoza.
- **Stadi za Mawasiliano** lengo lake kuu ni kufanikisha kufika ujumbe uliokusudiwa kwa walengwa ili kufanikisha kilichotakiwa kutekelezwa. Kukosea katika kutoa maelekezo, au matumizi ya maneno au mwonekano wa uso na kusababisha ulichosema kisieleweke, yote haya ni miongoni mwa yanayojadiliwa katika mada hizi.
- **Ubunifu na Vitendea Kazi** lengo lake ni kuelimisha jinsi wanavyojifunza elimu kwa njia mbalimbali ili kurahisisha uelewa wa kilichokusudiwa. Kwa kuelewa utofauti huu, ubunifu wa kuboresha uelewa kwa njia ya vitendea kazi mbalimbali kwa kutegemeana na aina za watu, wakati na mahali, huwa muhimu kwa kiongozi kujua na kujijengea uwezo.
- **Uinjilisti wa Watoto** ni mada iliyongezeka kama mpya safari hii. Kadri tunavyosogelea mwisho wa wakati kiunabii, huduma ya watoto kiinjilisti itazidi kupata nguvu zaidi na kueleweka vizuri masikioni mwa watu wazima, (Yoel 2:28-31 na Math 21:14-16). Eneo hili linahitaji uboreshaji zaidi.

2. **Pata au uwe na Nishani zifuatazo**:

   a. Masimulizi ya kikristo
   b.Stadi za Ukambikaji , hatua ya 1-IV
   c. Elimu ya Msingi juu ya Kwata na Parade
   d.Mafundo

- Mafunzo ya Nishani hutumia miongozo ya Nishani kimakundi kwa kufundishwa na mwalimu aliyeidhinishwa

na Mkurugenzi wa Konferensi kwa kusudi hilo.

3. **Pata Nishani mbili zaidi au Tuzo mbili zaidi za uchaguzi wako ambazo ulikuwa hujapata huko nyuma.**
   - Elimu kwa njia ya Nishani imegwanywa katika makundi 8 yafuatayo:
     1) Sanaa na Kazi za Mikono (Arts and Crafts).
     2) Afya na Sayansi ya Usafi (Health and Science)
     3) Sanaa za Nyumbani (Household Arts)
     4) Viumbe vya Asili (Nature Study)
     5) Uchumi wa Nje (Outdoor Industries)
     6) Huduma za Uinjilisti
     7) Maburudisho (Recreation)
     8) Stadi za maisha (Vocations)
   - Chini ya kila kundi kuna nishani nyingi zinazompatia mwanfunzi ujuzi tofauti tofauti katika Nyanja hiyo. Mwanafunzi anapopata nishani aina 7 tofauti tofauti chini ya kundi moja ndipo hustahili kupewa ile iitwayo "Master" katika kundi hilo. Mfano: Artsan Master- ana nishani 7 katika kundi la sanaa na kazi za mikono; au "Recreation Master"- ana nishani 7 katika kundi la maburudisho.
   - Nishani sio mapambo au urembo kwenye mikanda. Uchaguzi wa nishani za kusoma uzingatie kuweka uwiano wa ujuzi unaowezesha kutumika katika Nyanja zote ili kufaa zaidi kuieneza injili kwa kutumia uzoefu tofauti tofauti wa kielimu.
4. **Pata cheti cha wakati huu cha msaada wa kwanza, cha Red Cross, au Cheti cha Usalama, (Safety Certificate) au huduma inayotimiza hitaji hilo**.
   - Kipindi cha chini cha Kozi hii ni masaa 12. Kusudi la hitaji hili ni kumwezesha mwanafunzi kutambua mabadiliko ya kiafya mwilini na jinsi ya kukabiliana nayo hasa yanyohusiana na: upumuaji, kutokwa na damu na jinsi inavyoweza kuzuiwa kidharura, jeraha zitokanazo na kuungua moto, mikato mikali, joto kali au baridi kali, na dharura zitokanazo na kuhudumia vidonda, na wagonjwa wa kisukari, au kula vitu vyenye sumu.
   - Aidha kozi hii pia hushughulikia mishtuko ya ghafla inayoweza kuwapata vijana kama matokeo ya hofu; kuanguka na kuteguka au kuvunjika na mengineyo yanayofanan na hayo.
5. **Kwa kipindi kisichopungua mwaka moja shiriki kusimamia**

**huduma vijana wadogo katika darasa mojawapo la Wavumbuzi au Watafuta Njia au fundisha darasa la Shule ya Sabato kwa watoto wa umri wa miaka 6-15.**

- Kanisa mahalia limchague kutumika kama mwanafunzi mafunzoni ili akamilishe kozi yake ya uongozi. Endapo nafasi zitakuwa zimejaa, Vyama vya Wavumbuzi na Watafuta Njia vimpatie kazi ya kufanya ili akamilishe hitaji hili, ikiumbukwa kuwa kpindi cha juu cha kuchukua kozi hii ni miaka 3. Kama atakuwa anaanza mwaka wa mwisho wa 3 na hitaji hili lisitimizwe ni wazi ucheleweshwaji utajitokeza unaoweza kumfanya asihitimu tena maana amevusha miaka 3.

## IV. <u>MAENDELEO YA MTOTO</u>

1. **Soma au usomewe kitabu cha: "Education", (Elimu ya Kweli)cha E.G. White, na uandike na kukabidhi ufupisho wa ukurasa mmoja wa mambo uliyonufaika nayo kutokana na usomaji huo**.
   - Kitabu hiki kwa sasa kinapatikana kwa lugha ya Kiswahili kwa jina la "Elimu ya Kweli". Kinaelezea masuala mengi ya kufanikisa elimu yenye lengo la kubadili tabia ya mtu, kikieleza miongozo ya kufundishia elimu ilivyo na fasafa mbalimbali ya jinsi wanadamu wanavyotakiwa kujifunza au kufundishwa elimu, wadogo kwa wakubwa. Hii miongozo na falsafa ndiyo tunayomtegemea msomaji agundue na aeleze jinsi anavyoitumia na atakavyoboresha ufundishaji wake kwa kuitumia.
2. **Soma au usomewe kitabu kingine juu ya maendeleo ya mtoto,kati ya Child Guidance, au Messages to young People vyote vya E.G White, na uandike na kukabidhi ufupisho wa ukurasa mmoja wa mambo uliyojifunza na jinsi ulivyonufaika nayo.**
   - Vitabu hivi, ambavyo vyote vimeandikwa na Ellen G White, vimelenga kufundisha mambo mengi yakiwemo maadili kwa vijana na watoto yanavyotakiwa kujengwa. Msomaji atakutana na Kanuni muhimu za malezi na uwajibikaji katika maisha. Kanuni hizi na msisitizo wa maadili uluiotolewa ndivyo tunavyomtegemea msomaji avigundue na kuvitumia maishani ili kuonesha jinsi alivyo nufaika.
3. **Hudhuria semina tatu zinazojadili maendeleo ya mtoto wa umri unaohudumia, au semina za kielimu zihusianazo na**

**umri halisi wa mtoto unashughulika naye**.

- Tunajielimisha kwa njia mbalimbali, lakini zilizo kuu ni kuona, kusikia, kugusa/kushiriki. Kuhudhuria mikutano hutuongezea uzoefu wa kuona, kusikia na kugusa na kugundua mapungufu yetu kisha kuchukua hatua za kuboresha huduma zetu. Hii ndiyo maana ni muhimu kumtaka mwanafunzi ahudhurie semina zaidi ya kukaa ofisini kwake na kujisomea vitabu vyake tu.

4. **Kwa muda wa masaa 2 chunguza shughuli zifanywazo na Wavumbuzi au Watafuta Njia na uandike ulichogundua kutokana na shughuli zilizokuwa zinafanyika**.
   - Kinachofanyika hapa sio kusimamia shughuli bali ni uchunguzi wa jinsi shughuli zinavyofanyika. Zoezi hili linahusisha mambo kadhaa yakiwemo yafuatayo: (1) Kuielewa shughuli inayofanyika, (2) Kuelewa jinsi shughuli inavyofanyika, (3)Kuwaelewa wanoifanya hiyo shughuli, kwa jinsia zo na idadi yao, (4) Kuelewa kama watendaji wana msimamizi au hawana, (5) Kuelewa kinachofanikishwa na shughuli inayofanyika, (6) Kutathmini morali ya kazi ilivyo kadri muda unavyopita wakiwa kazini, n.k. Uchungaji huu humpatia kiongozi kugundua uwajibikaji kazini na jinsi ya kuuboresha. Aidha humpatia kuwajua watendaji na uwezo wao na motisha wanazohitaji ili kufanikisha malengo ya chama.

## V. <u>KUJIENDELEZA KATIKA UONGOZI</u>

1. **Soma kitabu kinachozungumzia kujiendeleza katika stadi za uongozi katika ujumla wake cha uchaguzi wako miongoni mwa orodha iliyopendekezwa hapa:**
   a. Positive Church in a Negative World, John Arrias
   b. Take the Risk, Ben Carson
   c. Ellen White on Leadership by Cindy Tutsh
   d. Help! I'm being Followed by Clinton Valleyn
   e. Other book recommended by your Conference/ Mission,
   Youth Ministries Director
   - Orodha ya vitabu vilivyotajwa hapa juu kubwa ni ya kimagharibi**.** Kila kukicha vitabu vinaandikwa kuhusu uongozi na jinsi ya kuuboresha. Vitabu vilivyokuwa vizuri kipindi fulani sasa havipendelewi tena, hivyo huwa vigumu kusema hiki ndiko kitabu cha kwanza kwa ubora katika

kuelezea uongozi. Hata hivyo kam utaweza kupata mojawapo ya nakala hizo juu waweza tumia.

- Vitabu hivi vikikosekna kanisani shauriana na Mkurugenzi wako wa Konferensi akupendekezee miongoni mwa vitabu vilivyo sokoni vinavyopendekezwa na Kanisa mahali mlipo. Kitabu cha: “ **Leadership Is an Art**” kilichoandikwa na **Max dePreez**, ni miongoni mwa vitabu vilivyopendekezwa katika mtaala uliopita wa Kozi hii ya Kiongozi Mkuu. Kama ulikuwa hujakisoma ni vizuri kukisoma pia.

2. **Dhihirisha kuwa na stadi zako za uongozi kwa kufanya yafuatayo**:

a). Andaa na uendeshe ibada 3 kwa watoto na au vijana wanaobarehe, za ubunifu wako mwenyewe

b). Shiriki katika Kambi au mkutano wa Vijana ngazi ya Konferensi, wewe ukiwa na watoto wa kanisani kwako ukitumika kama mmojawpo wa viongozi wao

c). Fundisha tuzo tatu za Wavumbuzi au Nishani mbili za Watafuta Njia

d). Saidia katika kupanga na kuongoza safari ya mafunzo ya Wavumbuzi, Watafuta Njia au darasa la Shule Sabato lenye umri kati ya miaka 6-15, iliyofanyikia nje ya Kanisa

e). Uwe miongoni mwa maofisa wachapa kazi wa Chama cha Wavumbuzi, Watafuta Njia, au wa shule ya sabato, kwa mwaka mmoja na uhudhurie angalau asilimia 75 ya mikutano ya viongozi.

- Kushiriki ni zaidi ya kuhudhuria tukio kama mmojawapo wa wajumbe. Ni kujishughulisha katika tukio hilo.
- Kinachohitajika kujulikana katika kushiriki ni kuandaa taarifa ya mkutano huo na jinsi wewe ulivyotumika katika nafasi mbalimbali kwa kila moja la matano yaliyo orodheshwa juu.Ni kutoa taarifa ya jinsi kila moja katika hayo lilivyotekelezwa. Kama ni kambi au mkutano aeleze: Ni wapi? Lini? Kusudi lilikuwa ni kufanikisha nini? Yeye alishirikije kufanikisha hilo kusudi? Kama ni ufundishaji wa Nishani au semina, kabidhi nakala ya kitini ulichotumia kufundishia, ikiambatana na idadi iliyofundishwa, waliofuzu, changamoto ulizokutana nazo na jinsi ulivyozikabili.

- Kwa kifupi kinachofanyika katika kila moja la haya matakwa matano ni kutoa taarifa ya jinsi ulivyoshiriki na matokeo ya kushiriki kwako katika tukio husika.

3. **Andika malengo makuu unayohitaji kuyatimiza katika huduma yako.**
   - Itambue huduma yako, kama ni ya Watafuta njia au ya Wavumbuzi. Tambua kipindi cha huduma yako, kama ni miaka 3 au 5 au zaidi. Tambua unaohudumia na unaohudu nao. Baada ya utambuzi huo sasa andika angalo malengo 3 unayotaka kutimiza katika huduma hiyo kwa kipindi husika.
4. **Tambua majukumu matatu ya sasa katika maisha yako,mojawapo likiwa ni la kiroho kisha kwa kila jukumu orodhesha malengo madogo 3 unayotaka kufanikisha**.
   - Kusudi la zoezi hili ni kumsaidia mwanafunzi kuwa na mwelekeo unaojulikana maishani maana mwanadamu haishi kwa bahati bali kwa kupangilia mambo na vipindi vya kuyatekeleza.
   - Kushindwa kuyaona maisha katika mpango na kinachofanikishwa na mpango huo ni udhihirisho wa kuishi

     bila malengo na yumkini kuongoza vijana wadogo bila malengo. Kila kiongozi anategemewa afanikishe hili takwa kwa uzuri kabisa maishani mwake.
   - Msisitizo wa kiroho umetajwa. Kukua kiroho, au kujizoeza katika utauwa ni matendo ya imani yanayochaguliwa na mwanafunzi, ili maisha yake yawe kielelezo cha kuigwa na vijana wake.

## VI. <u>KUJIENDELEZA KIAFYA</u>

1. **Kuza afya ya viungo vyako kwa kukamilisha mojawapo ya yafuatayo**:
   a. Kamilisha tuzo ya AY ya Silver Award na kama unayo tayali, kamilisha tuzo ya AY ya Gold Award, zote zikihusika na mazoezi ya viungo
   b. Shiriki katika programu ya mazoezi ya viungo iliyoandaliwa na shule.
   c. Shiriki katika mpango maalumu wa mazoezi ya viungo uliouchagua kwa kuongozwa na kitabu cha mazoezi ya viungo , chini ya ushauri wa kiongozi wako.

- Kinachofuatiliwa hapa ni ulinganifu wa kuishi kiafya katika

ulaji, mazoezi, mavazi, mapumziko na nguvu za rohoni. Wengine huzidisha sana katika eneo moja na kupungua katika jingine. Semina za Afya na ulinganifu zitaendeshwa na kufuatiwa na utekelezaji wa kuboresha kuliko kuwa dhaifu.

- Msimamizi wa kozi akipenda kuona ratiba ya mazoezi ya kila wiki au kila siku hatakiwi kufichwa kuona unavyofanya mazoezi.
- Zoezi la kukabiliana na uchu wa chakula ni jingine la kupambana nalo. Ratiba yako ya kula kwa siku na kwa wiki ikoje? Ni nini kinacholiwa na kunywewa na kwa kiasi gani na kwa nini? Je ratiba hii inatiiwa kwa kiasi gani? Ni kiasi gani unapambana na uchu wa matumizi ya vyakula vyenye mafuta mengi, na sukari nyingi? Ni kwa kiasi gani unywaji wa maji umezidi unywaji wa juice? Kiongozi anatakiwa aonyeshe mfano kwa vijana anaowaongoza. Wakati wa mafunzo Menu yake yake ya chakula na vinywaji inatakiwa kuonekana jinsi alivyoiandaa, na anavyotumia elimu hiyo kuambukiza wengine wanaomzunguka, na hasa vijana wadogo.
- Unavaaje? Aina ya nguo kwa upande wa nyuzi za nguo zikoje? Nguo zinazosuguana na mwili nyuzi zake zina usalama kwa ngozi au zinaongeza madhara? Je Kanuni ya Walawi 19:19 inatimizwa kwa kiasi gani kuhusiana na uvaaji wa mavazi?

## VII. <u>TAARIFA/JARIDA LA MAFUNZO – DOCUMENTATION</u>

1. **Kwa ajili ya uhakiki wa mafunzo, Andaa na kabidhi Jarida (Portifolio), kuonyesha kila hitaji lilivyotimizwa kwa kuzingatia mahitaji yalivyoelekeza na jinsi lilivyofanyika**.

- Kozi ya Kiongozi Mkuu, sawa na kozi zingine za kuwahudumia vijana, kwa mujibu wa Mtaala hazina mtihani wa kufanywa kwa namna ya upimaji wa kikao kimoja cha maswali na majibu. Kinachofanyika ni kupima zaidi uelewa wa mwanafunzi kwa kuandaa taarifa ya alichojifunza kwa kukiweka katika maandishi anayoweza kuyaeleza na manufaa aliyopata kutokana na kujifunza masomo hayo. Mwanafunzi akishindwa kuonyesha masomo aliyosoma na jinsi yalivyomsaidia kujua jinsi ya kuwahudumia vijana wadogo unakuwepo wasiwasi kuwa kule kusainiwa kwenye kadi lake kumekaa kimtihani zaidi badala ya kimaarifa yatumikayo. Hivyo mwanafunzi asihitimishwe bila hili Jarida kuonekana likiwa ni utendaji wake mwenyewe.

**<u>Kiambatanisho- 3</u>: <u>FOMU YA TAARIFA YA HUDUMA ZA IDARA KILA ROBO – ( Sahihisho la 2016)</u>**

# SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH, NORTHERN TANZANIA UNION CONFERENCE

# YOUTH MINISTRIES DEPARTMENT BI-ANNUAL REPORT: TAREHE ILIYOTUMWA__________

Confer________Churches ________ Companies _______

Membership _________Number of Youth (4-30+) ____

| | Vijana Wadogo (6 -15) | | Vijana Wakubwa, (16-30++ | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya: | A.C (6-9) | PFC (10-15) | A.M.C, (16-21) | Y/Adults, (22-30+) | |
| **MUUNDO** | | | | | |
| Vyama Vilivyopo | | | | | |
| Wanachama Waliopo | | | | | |
| Wanachama waliobatizwa | | | | | |
| Kwaya za Vijana zilizopo | | | | | |
| **MAFUNZO YA UONGOZI** | | | | | |
| Walioseminishwa, ( wengineo) | | | | | |
| Wachungaji/Wazee/ Washauri waliopata mafunzo | | | | | |
| **Wahitimu M/Guide Waliopo** | | | | | |
| **Wahitimu K/ Mwadventista Waliopo** | | | | | |
| **AYMT Waliotuzwa** | | | | | |
| **KUJITOA** | | | | | |
| Wanachama waliobatizwa | | | | | |
| Wanachama walioongezeka | | | | | |
| Waliovishwa pini + Vyeti (AMC) | | | | | |
| Waliovishwa Nishani | | | | | |
| **UANAFUNZI** | | | | | |
| Wanaosoma Biblia kwa Mpango | | | | | |
| Wanaosoma Kesha la Asubuhi | | | | | |
| Wasoma Vitabu vya Roho/Unabii | | | | | |
| Wasoma Vitabu vilivyoagizwa | | | | | |
| **KUSHUHUDIA** | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Mradi wa Eliya | | | | | |
| Matumizi ya Miradi ya Mahubiri | | | | | |
| Uinjlisti kupitia Huduma za Jamii | | | | | |
| Miradi mingine ya Uinjilisti | | | | | |
| Vijana walioshiriki Uinjilisti | | | | | |
| Waliobatizwa kwa Ushuhudiaji | | | | | |
| **USHIRIKA** | | | | | |
| Mikutano ya Idara:Rale/ Kongresi/Camporee/Retreat/n.k | | | | | |
| Mikutano ya Vikosi/Vyama:Makambi, n.k | | | | | |
| **KUJITEGEMEA** | | | | | |
| Mafunzo ya Ujasiliamali | | | | | |
| Miradi ya kujitegemea iliyopo | | | | | |
| Watoa zaka/sadaka -wastani | | | | | |
| Watoa sadaka tu -Wastani | | | | | |

.

***NOTE:*** *Unaweza kutumia karatasi nyingine kuelezea miradi ilivyofanyika au taarifa ya ziada unayohitaji tujue, zikiwemo picha za matukio, na makundi ya vijana yaliyotekeleza: Mfano: Young Pfrossionals; Singles; Young cpuples,n.k*

**Youth Director's Name ____________________ Signature______________________**

# SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH, NORTHERN TANZANIA UNION CONFERENCE

# YOUTH MINISTRIES DEPARTMENT BI-ANNUAL REPORT: DATE SENT________

Confer__________Churches __________Companies ________

Membership _____________ Number of Youth (4-30+) ___

| | **JUNIOR YOUTH (6-15)** | | **SENIOR YOUTH (16-30++++)** | | **TOTAL** |
|---|---|---|---|---|---|
| Number of: | A.C (6-9) | P.F.C (10-15) | A.M.C (16-21) | Y.A (22-30) | |
| **ORGANIZATION** | | | | | |
| Clubs organized | | | | | |
| Members by club | | | | | |
| Baptized members by club | | | | | |
| AYM Choirs | | | | | |
| **LEADERSHIP TRAINING** | | | | | |
| Participants of General Leadership Training | | | | | |
| Pastors, Elders & Sponsors trained in AYM | | | | | |
| Invested Master Guides Present | | | | | |
| Invested Youth Leadership Masters Present | | | | | |
| Certified AYMT | | | | | |
| **COMMITMENT** | | | | | |
| Newly baptized members | | | | | |
| Inducted members | | | | | |
| Invested/Certified members (+ Modules) | | | | | |
| **DISCIPLESHIP** | | | | | |
| Participants in Bible/Encounter Y/ Program | | | | | |
| Observers of Morning Watch | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Spirit of Prophecy books readers | | | | | |
| Book reading clubs Registered | | | | | |
| **WITNESSING** | | | | | |
| Project Campaigns*- | | | | | |
| Projects Campaigns*- | | | | | |
| Community impacts (outreach) | | | | | |
| Other soul winning projects done | | | | | |
| Youth involved in these activities | | | | | |
| Baptisms of new converts | | | | | |
| **FELLOWSHIP** | | | | | |
| AYM Retreats/Congresses/ Festivals/camps | | | | | |
| Sub-Groups retreats/camps** | | | | | |
| **SELF-SUPPORT** | | | | | |
| Training on Entrepreneurship | | | | | |
| Self-Support Projects | | | | | |
| Tithe and Offering Returnees | | | | | |
| Offering Returnees only | | | | | |

*Mention the project; **these are groups such as: Young Professional, Young Couples, Singles, etc.*

***NOTE:*** *Use a different sheet to give any more detailed report. Attach photos when applicable and possible*.

**Youth Director's Name______________________________, Signature_________________________**

EAST- CENTRAL AFRICA DIVISION – YOUTH MINISTRIES DEPARTMENT

**YOUTH MINISTRIES DEPARTMENT BI-ANNUAL REPORT (MAR. 15 & SEPT. 15), DATE______________**

Union___________, Total Membership__________ Total number of Youths (4-30)_____________

| | **JUNIOR YOUTH (6-15)** | | **SENIOR YOUTH (16-30++++)** | | **TOTAL** |
|---|---|---|---|---|---|
| Number of: | A.C (6-9) | P.F.C (10-15) | A.M.C (16-21) | Y.A (22-30) | |
| **ORGANIZATION** | | | | | |
| Clubs organized | | | | | |
| Members by club | | | | | |
| Baptized members by club | | | | | |
| AYM Choirs | | | | | |
| **LEADERSHIP TRAINING** | | | | | |
| Participants of General Leadership Training | | | | | |
| Pastors, Elders & Sponsors trained in AYM | | | | | |
| Invested Master Guides Present | | | | | |
| Invested Youth Leadership Masters Present | | | | | |
| Certified AYMT | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **COMMITMENT** | | | | | |
| Newly baptized members | | | | | |
| Inducted members | | | | | |
| Invested/Certified members (+ Modules) | | | | | |
| **DISCIPLESHIP** | | | | | |
| Participants in Bible/Encounter Year Program | | | | | |
| Observers of Morning Watch | | | | | |
| Spirit of Prophecy books readers | | | | | |
| Book reading clubs Registered | | | | | |
| **WITNESSING** | | | | | |
| Project Campaigns*- | | | | | |
| Projects Campaigns*- | | | | | |
| Community impacts (outreach) | | | | | |
| Other soul winning projects done | | | | | |
| Youth involved in these activities | | | | | |
| Baptisms of new converts | | | | | |
| **FELLOWSHIP** | | | | | |
| AYM Retreats/Congresses/ Festivals/camps | | | | | |
| Sub-Groups retreats/camps** | | | | | |
| **SELF-SUPPORT** | | | | | |
| Training on Entrepreneurship | | | | | |
| Self-Support Projects | | | | | |

*Mention the project; **these are groups such as: Young Professional, Young Couples, Singles, etc.*
***NOTE:*** *Use a different sheet to give any more detailed report.*

*Attach photos when applicable and possible.*

**Youth Director's Name______________________________,**
**Signature_________________________**